# UNIVERSITY JOURNAL

*ISSN: 2507-7864*

## EDITORIAL BOARD

| | |
|---|---|
| Prof.Yunis Abdille MUSA | Chief Editorial Board |
| Prof. Fowzi Mohamed Barrow | Editor |
| Prof.Msafiri Mshewa | |
| Prof.Mohamed Ali El-Kamil | |
| Mr.Burhan Hatinbu muhuzi | |
| Mr. Mohamed Haji Ali | |
| Mrs.Mwanatumu Ali Hassan | |

Advisor Board

| | |
|---|---|
| Prof. Amran Mohamed Rasli | (Chairman) SUMAIT University |
| Prof. Hamed Rashid Hikmany | SUMAIT University |
| Prof. Mustafa Adam Rushash | Zanzibar University |
| Prof. Said Ahmed Moh'd. | The State University of Zanzibar |
| Prof. Mohammed Al sheikh | The State University of Zanzibar |
| Dr. Miraji Ukuti Ussi | Commission for tourism, Zanzibar |
| Dr.Nassor Hamad Bakari | SUMAIT University |
| Dr. Mohamed Saleh Abdala | SUMAIT University |

**The Chief Editor,**
**SUMAIT University Journal of Scientific Studies,**
**P.O. Box 1933,**
**Zanzibar, Tanzania**
**Ph. +255-24-223-9396**
**E-mail:** sumaitcrpc@gmail.com
**Website: http://www.sumait.ac.tz**
**Annual Subscription: USD 5 (2 issues) for institutions,And USD 40 (2 issues) for individuals**

**ISSUE NO:5 DECEMBER 2018**

# UHUSIANO WA MOFU ZA NJEO KATIKA KITENZI CHA KITUMBATU NA KISWAHILI SANIFU

**Ulfat Abdull-aziz Ibrahim**♥

## Abstract

This article focuses on the field of Morphology in examining the relationship between morphemes that represent aspects in a verb structure of Standard Kiswahili and Kitumbatu (dialect) as well as identifying the impact that arises because of that relationship. This study highlights some of the verbs from Kiswahili Standard and Kitumbatu and examines them through their internal and external structures. The article identifies the similarities and differences between the Kiswahili and the Kitumbatu verbs due to their representation of the affixes (morphemes of aspects). Among the areas that appear to be the same are in the morphemes of present tense that are represented by the morph (-na-) in affirmative case. Differences are also seen in the morphemes of past tense in the status of affirmative. The study also identifies the effects of the similarities or variations of those morphemes of aspects. Among these are the effects of phonological processes emerging from various principles including the principle of vowel harmony. From this study we can conclude that there is an interrelation between Standard Kiswahili and Ktumbatu dialect, since there are similarities and even differences in the affixes (morphemes of aspects) in use.

## Ikisisri

Makala hii imejikita katika taaluma ya Mofolojia kwa kuchunguza uhusiano wa mofimu za njeo kwenye muundo wa kitenzi katika Kiswahili Sanifu na Kitumbatu pamoja na kubainisha athari zinazojitokeza kutokana na kuwiana kwa mofimu hizo. Utafiti huu uliangazia baadhi ya vitenzi kutoka katika Kiswahili Sanifu na Kitumbatu na kuvichunguza kupitia muundo wa ndani na muundo wa nje wa vitenzi hivyo. Makala hii imebaini kuwiana na kutofautiana baina ya vitenzi vya Kiswahili Sanifu na Kitumbatu kutokana na viambishi vyao vinavyowakilisha njeo. Miongoni mwa sehemu ambazo zinaonekana kuwiana ni katika mofimu ya njeo ya wakati uliopo katika hali ya uyakinishi ambayo huwakilishwa na mofu (-na-). Aidha utofauti unaonekana katika mofimu ya njeo ya wakati uliopita katika hali ya uyakinishi. Utafiti huu umebainisha athari zinazotokana na kufanana au kutofautiana kwa mofimu hizo za njeo. Miongoni mwa athari hizo ni kujitokeza kwa michakato ya

♥ Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Luqhawiya,Chuo Kikuu cha Abdulraman Al- Sumait,Zanzibar

kifonolojia kwa kujitokeza kanuni mbalimbali ikiwemo kanuni ya tangamano la irabu (TI).Hivyo basi kutokana na utafiti huu tunaweza kusema kwamba kuna muathiriano kati ya lugha hizi mbili, kwani kuna kufanana na hata kutofautiana kwa viambishi (vya njeo) katika matumizi.

## 1.0 Utangulizi

Tunaweza kubaini tofauti ya matumizi ya lugha katika uzungumzaji wa kikundi cha watu fulani katika maeneo maalumu na uzungumzaji huo ukatofautiana na kikundi kingine kinachoishi katika maeneo mengine. Tofauti za uzungumzaji huo zinaweza kuwa za kimofolojia, kifonolojia au kimsamiati.

Katika makala hii mwandishi anazungumzia mambo mbalimbali ili kukidhi lengo la kuisambaza elimu hii kwa wasomaji ili wawe pamoja na naye katika kubaini kile ambacho amelenga kukibainisha kwa watu. Mambo yanayozungumziwa katika makala hii ni pamoja na dhana za lahaja, mofimu, mofu, uhusiano wa mofimu za njeo katika kitenzi cha Kiswahili Sanifu na Kitumbatu. Mwisho mwandishi anabainisha athari mbalimbali zinazotokana na uhusiano huo.

## 2.0 Maelezo kuhusu dhana mbalimbali

### 2.1 Dhana ya Lahaja

Kwa mujibu wa Crystal (1997), lahaja ni mtindo bainifu wa lugha kieneo na kijamii unaobainishwa na seti maalumu za maneno na miundo ya kisarufi. Kwa maelezo haya kipengele cha mtindo bainifu wa lugha kimefafanuliwa na Ng’waje (2016) kwa kusema:

“…neno mtindo katika fasili ya Crystal halisadifu kwani mtindo katika lugha unaweza kuwa wa watu fulani tu ndani ya jumuiya ya lugha na wakati mwingine ukihusisha rika fulani tu la watu, (mfano vijana, wanawake n.k)… Lahaja haina ubaguzi wa Kijinsia, rika na kadhalika.”

Aidha, Massamba (2002), amesema kwamba lahaja ni lugha mbalimbali za pwani zilizokuwa na uhusiano wa karibu sana. Lahaja hizo ni kama vile Kimbalazi, Kiamu, Kimvita, Kijomvu, Kimtang’ata, Kimakunduchi, Kiunguja mjini, na Kitumbatu.

Kutokana fasili hiyo tunaweza kuzieleza lahaja za Kiswahili kuwa hutofautiana kulingana na maeneo yake kama Kiunguja Mjini ( kisiwani Unguja) Kimvita (eneo la Mvita au Mombasa mjini, Kenya), Kitumbatu (kisiwa cha Tumbatu) n.k.

Pamoja na maelezo ya wataalamu waliotangulia, tunaweza kuelezea lahaja kuwa ni utofauti wa utumiaji wa lugha moja ambao hujipambanua kwa sifa za kiisimu na hata za kiarudhi kulingana na umbali wa kimaeneo kwa wanajamii wanaotumia lugha hiyo.

## 2.2 Kiswahili Sanifu

Lahaja sanifu (lugha sanifu) ni lahaja ambayo imeteuliwa kutoka lahaja nyingine kutumika kwa upana zaidi kuliko lahaja za kawaida. Hufanyiwa marekebisho katika matamshi, sarufi au hata semantiki na hutumika katika mawasiliano yaliyo rasmi.

Usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ulianza tangu mwaka 1930 ilipoundwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki. Suala la msingi ilikuwa ni kuteuliwa lahaja mojawapo ya lugha ya Kiswahili katika lahaja takriban kumi na tano. Kwa kuzingatia kuwa lahaja ya Kiunguja ilikuwa imeenea katika sehemu kubwa, ndipo ikapata nafasi ya kuteuliwa ili iweze kusanifishwa.

Baada ya Vita Vikuu vya Kwanza, Serikali ya Kikoloni iliunda Kamati ya Lugha kwa madhumuni ya kuunda Kiswahili sanifu kitakachotumiwa kote Afrika ya Mashariki. Hapo ndipo kilipopatikana Kiswahili Sanifu. http://www.mwananchi.co.tz/swahilihub/makala/2655370-2658508-885gy4/index.html

## 2.3 Lahaja ya Kitumbatu

Lahaja hii inazungumzwa katika Kisiwa cha Tumbatu. Kisiwa cha Tumbatu ni

sehemu ya wilaya ya Kaskazini “A” Zanzibar. Kisiwa hiki kipo kaskazini-

Magharibi ya kisiwa cha Unguja karibu na ghuba ya Mkokotoni. Kuna jamii kuu mbili katika kisiwa cha Tumbatu: Gomani/Kichangani na Jongowe. Watumbatu hujihesabu kama Washirazi waliokuwa na tawala zao ambazo ziliruhusu wanawake kutawala.

Stude (1995:94) anaripoti kuwepo kwa idadi ya watu wapatao 7,971 kwenye jamii hizo kuu mbili. Kitumbatu kimeshabihiana sana na lahaja izungumzwayo katika kijiji cha Nungwi nje kidogo ya Unguja-mjini upande wa Kaskazini (Kipacha 2003).

## 2.4 Dhana ya mofimu

Kwa maelezo ya Massamba na wenzake (2001), mofimu ni kipashio kidogo kabisa chenye uamilifu wa maana katika maumbo ya maneno.

Fasili hii imebainisha mambo mawili ya msingi katika dhana ya mofimu. Jambo la kwanza mofimu ni kipashio kidogo kabisa katika maumbo ya maneno na jambo la pili ni maana inayotokana na kipashio hicho kidogo. Hivyo basi tunaweza kusema kwamba mofimu ni sehemu ndogo zaidi ya neno inayowakilisha maana ya neno hilo. Mofimu ni dhana dhahania, hudhihirika kupitia mofu.

Mofimu kupitia mofu inaweza kuwa silabi moja au zaidi. Kwa vile mofimu inaweza kuwa silabi moja mfano ‘ki’ katika neno kiti au ‘vi’ katika neno viti, tunajifunza kuwepo kwa uamilifu wa kisarufi. Vile vile katika silabi zaidi ya moja ambapo tunazungumzia neno, napo pia tunajifunza uamilifu wa kimsamiati. Kwa hivyo mofimu tunaweza kuzigawa katika aina mbili ambazo ni mofimu huru na mofimu tegemezi.

**Mofimu huru:** Mofimu huru ni silabi moja au zaidi yenye maana kamili ya neno na inaweza kujisimamia yenyewe bila msaada wa viambishi au silabi nyingine. Aghalabu mofimu huru huwa nomino, vivumishi au vielezi visivyochukua viambishi vya ngeli.
Kwa mfano: daftari, kalamu, nyumba.

**Mofimu funge/tegemezi:** Mofimu tegemezi ni mofimu ambazo huhitaji viambishi au mofimu nyingine tegemezi ili kuleta maana iliyokusudiwa. Mofimu hizi hujumuisha hasa mzizi wa neno (au shina la kitenzi), vivumishi, nomino au vielezi ambavyo vinahitaji viambishi viwakilishi vya ngeli ili kutoa maana iliyokusudiwa.

kwa mfano;

**mchezaji** =>m-chez-a-ji
{**m** => mofimu ya ngeli ya M-WA kwa umoja
**chez**=> mzizi wa neno, kiini cha kitendo cha kucheza
**a** =>kiishio cha kitenzi
**ji** => inaonyesha kazi au mazoea (Massamba na Wenzake 2003).

**2.5 Dhana ya mofu.**

Dhana ya mofu imeelezwa na wataalamu mbalimbali. Habwe na Karanja (2007:75) wanaelezea dhana ya mofu kwa kigezo cha kisarufi ni maana itokanayo na uamilifu wa kisarufi na kwa kigezo cha kileksia hurejelea maana ya neno likiwa peke yake kama linavyofahamika kwa watumiaji wa lugha inayohusika.

Massamba na wenzake (2004), wamesema kwamba mofu ni umbo linalowakilisha mofimu katika maandishi. Vile vile mofu ni kipashio cha kimaumbo (kimofolojia) kinachowakilisha mofimu, Massamba na wenzake (2003).

Kutokana na fasili hizo, tunaweza kusema kwamba mofu ni kipashio kinachofanya kazi kwa niaba ya mofimu. Ikumbukwe kwamba mofimu ni kitu ambacho ni dhahania; kwa hiyo kinachoonekana ambacho kinabeba dhima ya mofimu ni mofu. Kipashio kinachowasilishwa kimaandishi na kinaonekana kwa uwazi na kwa udhahiri, ndio tunachokiita "mofu".

Kwa mfano:

a- na- som -a

1 2 3 4

a- mofu inayowakilisha mofimu ya nafsi ya tatu umoja.

na- mofu inayowakilisha mofimu ya njeo ya wakati uliopo.

som- mofu inayowakilisha mofimu ya mzizi wa neno.

a- mofu inayowakilisha mofimu/kiambishi tamati kinachokalisha maana ya neno.

**2.6 Aina za mofu**

Tunaweza kuzigawa aina za mofu kwa kutegemea vigezo maalum. Kigezo cha maana ambayo imesitiriwa au kuwakilishwa na umbo hilo (mofu) na kigezo cha mofolojia ya mofu.

**2.6.1 Aina za mofu kwa kigezo cha maana zinazowakilishwa nazo**

Tunapotumia kigezo cha maana zinazowakilishwa na mofu, tunapata aina tatu za mofu, yaani; mofu huru/sahili, mofu funge/tegemezi na mofu tata. Kwa upande mwingine tunapotumia kigezo cha mofolojia au maumbo ya mofu zenyewe tunapata aina mbili za mofu, yaani; mofu changamano na mofu kapa. Hivyo, kwa kuanza na kigezo cha maana zifuatazo ni aina za mofu.

**Mofu huru/sahili:** Mofu huru ni umbo linalowakilisha mofimu huru; ni zile mofu ambazo zinaweza kukaa peke yake kama maneno kamili yenye maana inayoweza kueleweka bila kusaidiwa na mofu nyingine. Aghalabu, mifano mingi ya mofu huru

hupatikana kutoka kwenye vipashio vya lugha, kama vile nomino, vivumishi, viwakilishi na vyenginevyo. Mfano: Baba, ndege, dhaifu, hodari, mimi, sali .

**Mofu funge/tegemezi:** Mofu funge au mofu tegemezi ni maumbo yanayowakilisha mofimu tegemezi. Ni aina ya mofu ambayo haiwezi kutumiwa peke yake kama neno lililo na maana yake kamili; aghalabu mofu funge hutumiwa kama kiambishi tu kinachoambatanishwa na mzizi au viambishi vingine ili kulikamilisha neno husika. Sifa za mofu funge ni pamoja na:

- Mofu funge/tegemezi haiwezi kukaa peke yake ikawa neno kamili.
- Mofu funge/tegemezi ni lazima iambatanishwe na angalau mofu nyingine ndipo tuweze kuwa na neno kamili.
- Maana za mofu funge/tegemezi hutegemea sana muktadha wa mofu husika. Mofu funge/tegemezi ikiondolewa kwenye muktadha wake hukosa maana na ni vigumu kujua maana yake bila kuiweka katika muktadha wa neno.
- Mofu funge /tegemezi ni sawa na viambishi vya mizizi mbalimbali katika neno. Hii ina maana kwamba viambishi vilivyo vingi katika lugha huwa ni mofu funge/tegemezi. Tunasema viambishi vingi kwa sababu si viambishi vyote ambavyo huundwa kwa mofu funge. Mfano wa mofu funge ni viambishi vyenye maana ya umoja na wingi, viambishi vyenye maana ya wakati, viambishi vyenye maana ya mzizi/kiini n.k.

| Idadi ya Umoja | Idadi ya Uwingi |
|---|---|
| **m**-koba (m) | **mi**-koba (mi) |
| **k**i-ti (ki) | **vi**-ti (vi) |

Mmofu (-m-, -ki-,-mi-,-vi-) ni mofu tegemezi ambazo zimebeba maana ya idadi (umoja na wingi)

Mofu za njeo: Mofu za njeo ziko za aina tofauti kama zinavyojionesha hapo chini:

| | |
|---|---|
| A**na**soma- | (-na- )wakati uliopo |
| A**li**soma- | (-li -) wakati uliopita |
| A**ta**soma- | (-ta -) wakati ujao |
| A**me**soma- | (-me-) wakati timilifu |

Mofu (-na-,-li-,-ta-,-me-) ni mofu zinazowakilisha maana za nyakati tofauti.

**Mofu Tata:** Mofu tata huwakilisha mofimu ambazo zina maana zaidi ya moja. Ni mofu ambazo huwa na maana zaidi ya moja au kuanzia mbili na kuendelea. **Mfano**, Hadhra alimpigia Hanbal mpira.

Sentensi hii ni tata kwa sababu ina maana zaidi ya moja. Utata wa sentensi hii haupo kwenye muundo wake wa kisarufi, bali upo katika kitenzi **alimpigia**. Kitenzi hiki kina mofu sita, yaani:

| a- | -li- | -m- | -pig- | -i- | -a |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |

Kati ya mofu hizi zote sita, mofu ya tano (-i-) ndiyo yenye utata. Mofu (i) ni mofu ya kutendea kwa sababu tukisema: 'Hadhra **alimpigia** Hanbal mpira', maana zinazoweza kueleweka na wasikilizaji ni nne:

I. Hadhra aliupiga mpira **kwa niaba** ya Hanbal
II. Hadhra aliupiga mpira **kuelekea** kwa Hanbal
III. Hadhra alimpiga Hanbal **kwa kuutumia** mpira
IV. Hadhra alimpiga Hanbal **kwa sababu** ya mpira

Kutokana na maelezo na mfano tuliouelezea hapo tumebaini utata wa maana ambao umesababishwa na mofu (-i-). Kwa minajili hiyo mofu (-i-) ni mofu tata.

### 2.6.2 Aina za mofu kwa kigezo cha kimofolojia

Kwa kutumia kigezo cha mofolojia au maumbo ya mofu zenyewe, tunaweza kupata aina mbili za mofu kama zifuatazo:

**Mofu Changamani:** Mofu changamani ni maumbo ambayo yanawakilisha mofimu mbili . Ni mofu ambazo huundwa kwa kuweka pamoja angalau mofu huru mbili au mofu funge na mofu huru na kuunda neno lenye kuleta maana kamili; kwa mfano:

**Mofu huru + Mofu huru = Mofu changamani**

Bata + mzinga = batamzinga

Askari + kanzu = askari kanzu

**Mofu funge + Mofu huru = mofu changamani**

Mw- + -ana + nchi = mwananchi.

Ki-+ -ona + mbali = kionambali.

Kwa hiyo mofu changamani zinaweza kuundwa kwa mofu huru mbili kama ambavyo tulivyoona katika mfano wa kwanza. Vilevile inaweza kuundwa kwa mofu funge/tegemezi na mofu huru kama ambavyo ilivyoonekana katika mfano wa pili.

**Mofu Kapa:** Mofu kapa ni mofu za pekee ambazo hazina umbo. Kwa kawaida mofu kapa huwa hazitamkwi wala haziandikwi. Mofu kapa hazionekani katika neno, lakini athari zinazotokana na hiyo mofu kapa husika hueleweka. Ingawa mofu hizi huwa hatuzioni wala kuzitamka au kuziandika, lakini maana zake tunazipata. Hebu tuchunguze ruwaza ya viambishi awali vya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili ambazo tunaweza kuziona katika aina za majina. Nomino za Kiswahili zinaweza kugawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na maumbo yake ya umoja na wingi kama ifuatavyo;

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| u-nywele | **ø** -nywele |
| u - funguo | **ø** -funguo |
| **ø**-jembe | ma -jembe |
| **ø** -kasha | ma -kasha |
| **ø** -mama | **ø**-mama |
| **ø**-mbuzi | **ø**-mbuzi |

Nomino zinaweza kuwa na kiambishi kimoja tu au hata zisiwe na kiambishi (ø). Kiambishi hicho kinaweza kuonekana katika hali tofauti ikiwa ni hali ya umoja yaani (nomino za umoja) au wingi (nomino za wingi ) na nomino zisizo na kiambishi cha umbo la umoja wala wingi (ø)

Baada ya kudadavua dhana ya mofu, kwa upekee makala hii imejikita katika mofu tegemezi ambazo ni zile ambazo haziwezi kusimama pekee na kuweza kuleta maana pasi utegemezi wa mofu nyingine. Vile vile maana inatokana na muktadha

wake au uamilifu wake pale ambapo imejitokeza. Mofu za njeo ni miongoni mwa mofu zenye sifa hizo.

**3.0 Uhusiano wa mofu za njeo katika kitenzi cha kitumbatu na kiswahili sanifu.**

Katika kipengele hiki, makala imebainisha uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha kawaida(uyakinishi), uhusiano wa mofu ya njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha kawaida (ukanushi), uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati timilifu katika kitenzi cha Kiswahili sanifu na Kitumbatu (uyakinishi), uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati timilifu katika kitenzi cha Kiswahili sanifu na kitumbatu (ukanushi) pamoja na uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati uliopo katika kitenzi cha Kiswahili Sanifu na Kitumbatu (uyakinishi).

**3.1 Uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha kawaida (uyakinishi**)

Katika Kiswahili Sanifu kiambishi kinachotumika kuwakilisha wakati uliopita katika hali ya uyakinishi kwenye kitenzi cha kawaida ni (-li-). Kwa upande wa Kitumbatu hakitumiki kiambishi cha aina yoyote kuwakilisha njeo ya wakati uliopta, bali huainisha njeo ya wakati uliopita kwa kutumia kanuni maalumu. Katika mofofonimu kanuni hiyo inaitwa tangamano la irabu, ambalo ni mchakato wa kifonetiki ambao huhusu athari ya irabu moja kwenye irabu nyingine kiasi cha kuzifanya irabu hizo zielekee kufanana kabisa au kiasi katika sifa zake za kimatamshi (Massamba na wenzake, (2004).

Kwa ufupi tunaweza kusema kwamba katika Kiswahili Sanifu hutumika kipashio -li- kama mofu inayowakilisha mofimu ya njeo ya wakati uliopita, wakati katika Kitumbatu hutumika tangamano la irabu (TI). Utofauti huo unabainishwa katika mifano ifuatayo:

| **Kitenzi** | **Kiswahili Sanifu** | | **Kitumbatu** |
|---|---|---|---|
| Piga | ni-**li**-piga | = ni**li**piga | nip**igi** |
| Piga | Mu-**li**-piga | = mu**li**piga | mup**igi** |
| Cheka | tu-**li**-cheka | =tu**li**cheka | tuch**eke** |
| Soma | wa-**li**-soma | =wa**li**soma | was**o**m**o** |
| Nuna | a- **li**-nuna | =a**li**nuna | kan**u**n**u** |

### 3.2 Uhusiano wa mofu ya njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha kawaida (ukanushi)

Kwa upande mwingine tunaangalia uwiano wa kiambishi cha njeo ya wakati uliopita katika kitenzi cha kawaida (ukanushi). Kiambishi kinachotumika kuwakilisha njeo ya wakati uliopita katika hali ya ukanushi kwenye kitenzi cha kawaida katika Kiswahili Sanifu ni (-ku- ) na katika Kitumbatu hutumika kiambishi (-e-). Tazama mifano ifuatayo:

| **Kitenzi** | **Kiswahili Sanifu** | **Kitumbatu** |
|---|---|---|
| Piga | si-**ku**-piga =sikupiga | si-**e**-piga = s**e**piga |
| Cheka =hatw**e**cheka | ha-tu-**ku**-cheka=hatukucheka | ha-tu-**e**-cheka |
| Soma | ha-**ku**-soma =hakusoma | ha-**e**-soma =h**e**soma |
| Nuna | si-**ku**-nuna =sikununa | si-**e**-nuna =s**e**nuna |

### 3.3 Uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati timilifu katika kitenzi cha Kiswahili Sanifu na Kitumbatu (uyakinishi)

Kiambishi kinachowakilisha mofu ya njeo ya wakati timilifu (wakati uliopita muda/ kitambo kifupi) katika Kiswahili Sanifuni (-me-) na katika Kitumbatu ni (-ma-) katika hali ya uyakinishi. Tazama mifano ifuatayo:

Kiswahili Sanifu: a**me**sema hataki kukimbia

Kitumbatu: ka**ma**sema hataki kukimbia

Kiswahili Sanifu: a**me**kula sana

Kitumbatu: ka**ma**kula sana

Kiswahili Sanifu: a**me**lia sana

Kitumbatu: ka**ma**lia sana

### 3.4 Uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati timilifu katika kitenzi cha Kiswahili Sanifu na Kitumbatu (ukanushi)

Kwa upande wa ukanushi, Kiswahili Sanifu na Kitumbatu hutumia kiambishi cha aina moja cha (-ja/e-), kama inavyoonekana katika mifano hiyo.

Kiswahili Sanifu: mwanafunzi ha**ja**iba kitabu

Kitumbatu: mwanafunzi ha**je**ba kitabu

Kiswahili Sanifu: dada ha**ja**piga pasi

Kitumbatu: dada ha**ja**piga pasi

Kiswahili Sanifu: si**ja**uza kwa laki moja

Kitumbatu: si**ja**oza kwa laki moja

### 3.5 Uhusiano wa kiambishi cha njeo ya wakati uliopo katika kitenzi cha Kiswahili Sanifu na Kitumbatu (uyakinishi)

Kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopo katika Kiswahili Sanifu na Kitumbatu ni (-na-) kwenye hali ya uyakinishi, kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

| **Kitenzi** | **Kiswahili Sanifu** | **Kitumbatu** |
|---|---|---|
| Piga | ni**na**piga | n**a**piga |
| Imba | u**na**imba | ku**na**kwimba |
| Lia | tu**na**lia | tu**na**lia |

Katika kipengele hiki tumeona kwamba kuna kuwiana na kutofautina kwa mofu za njeo katika miundo ya vitenzi katika Kiswahili Sanifu na Kitumbatu. Hali hiyo imesababishwa na michakato ya kimofolojia kutokana na kuathiriana maumbo hayo.

## 4.0 Athari zilizojitokeza katika miundo ya vitenzi kutokana na michakato ya kimofolojia

Katika sehemu hii ya makala mwandishi amebainisha athari mbalimbali zinazojitokeza kutokana na michakato ya kimofolojia.

### 4.1 Michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya kimuundo kwenye kiambishi cha njeo ya wakati uliopita (uyakinishi):

Hapa tunaelezea michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya kimuundo wa ndani kwenda miundo ya nje kwenye kiambishi cha njeo ya wakati uliopita (uyakinishi).

Hakuna athari yoyote kwenye kitenzi cha Kiswahili Sanifu ambacho silabi yake ya mwanzo ni irabu pekee, kikiambikwa kiambishi (-li-) kinachowakilisha mofu ya njeo ya wakati uliopita. Lakini kwa upande wa kitumbatu athari ipo. Ni pale ambapo kanuni ya tangamano la irabu (TI) inapotumika kama alama ya kuonesha njeo ya wakati uliopita. Mifano katika hali ya uyakinifu:

| **Kitenzi** | **Kiswahili Sanifu** | **Kitumbatu** |
|---|---|---|
| Ita | ni-**li**-ita = niliita | ni-**iti** = n**yiti** |
| Acha | mu-**li**-acha =muliacha | muacha=m**wa**ch**a** |
| Ona | u-**li**-ona = uliona | ku-**ono =** k**ono** |

Katika mifano hiyo tumeona katika Kitumbatu hutumika kanuni ya TI kuwakilisha njeo ya wakati uliopita. Katika Kitumbatu hulazimika kuzikutanisha irabu mbili zinazofanana katika mpaka wa mofu.

**4.2 Michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya kimuundo kwenye kiambishi cha njeo ya wakati timilifu (uyakinishi):**

Hapa tunaelezea michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya muundo wa ndani kwenda miundo ya nje kwenye kiambishi cha njeo ya wakati timilifu (uyakinishi).

Tumekwishaona mifano katika kipengele cha uwiano wa mofu ya njeo ya wakati timilifu. Mifano ile inatoa ushuhuda juu ya matumizi ya kiambishi (-me-) katika Kiswahili Sanifu na kiambishi (-ma-) katika Kitumbatu kuonyesha njeo ya wakati timilifu. Mifano pia inaonyesha kwamba hakuna mabadiliko yoyote kwenye muundo wa ndani na muundo wa nje wa kitenzi. Hivyo basi viambishi hivyo katika tungo vinabaki kama vilivyo bila ya kupata athari ya aina yeyote katika mazingira yote ya uambikaji wa kiambishi njeo na kiambishi nafsi.

**4.3 Michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya kimuundo kwenye kiambishi (mofu) ya njeo ya wakati timilifu (ukanushi):**

Hapa tunaelezea michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya muundo wa ndani kwenda muundo ya nje kwenye kiambishi (mofu) ya njeo ya wakati timilifu (ukanushi).

Katika kiambishi cha njeo wakati timilifu katika ukanushi, kuna kiambishi (-ja-) katika Kiswahili Sanifu na Kitumbatu; mofu hiyo inabaki bila kubadilika kiambikwapo kwenye kitenzi cha muundo wowote kwenye Kiswahili Sanifu. Lakini mofu hiyo hujibadilisha na kuwa (-je-) kikikutana na kitenzi ambacho silabi yake ya mwanzo ni irabu ya /i/ au irabu ya /e/ katika lahaja ya Kitumbatu. Pia katika lahaja hiyo kiambishi (-ja-) hujibadilisha na kuwa (-jo-) kikikutana na kitenzi ambacho silabi yake ya mwanzo ni irabu ya /u/ au irabu ya /o/. Kanuni ya mvutano wa irabu hujitokeza pale ambapo kiambishi (-ja-) kinakutana na irabu /i/ na irabu/u/ katika mpaka wa mofu mbili. Wakati huo irabu /a/ huvutana na irabu /i/ au irabu /u/ na kukutana katikati kwenye nafasi ya irabu /e/ au /o/.

Kanuni hii ni mchakato wa kifonetiki ambao huhusu athari ya irabu moja kwenye irabu nyingine kiasi cha kuzifanya irabu hizo zielekee kufanana kabisa au kiasi katika sifa zake za kimatamshi (Massamba na Wenzake, 2003).

Kanuni hiyo kwa ufupi huwasilishwa kwa /a+i/ ⟶ /e/ au /a+u/ ⟶ /o/. Kulithibitisha hili, mtafiti amebainisha mifano iliyopo chini:

Kitumbatu: mnamsingizia, ha**je**ba.

Kiswahili Sanifu: mnamsingizia ha**ja**iba.

Kitumbatu: si**jo**za kwa laki moja.

Kiswahili Sanifu: si**ja**uza kwa laki moja.

Kiswahili Sanifu na Kitumbatu hutumia mofu (-ja-) kuwakilisha njeo ya wakati timilifu kwenye hali ya ukanushi ambapo vitenzi vya aina zote haviathiriwi na mabadiliko isipokuwa pale mofu (-ja-) kinapokutana na kitenzi kilichoanza na irabu /i,e,o,u/ kama silabi yake ya mwanzo kama ilivyo katika mifano iliyopita.

### 4.4 Michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya kimuundo kwenye kiambishi cha njeo ya wakati ujao (uyakinishi)

Michakato ya kimofolojia inavyoonyesha athari za mabadiliko ya muundo wa ndani kwenda muundo ya nje kwenye kiambishi cha njeo ya wakati ujao (uyakinishi).

Mabadiliko ya muundo wa kitenzi cha kawaida kwa wakati ujao katika hali ya uyakinishi katika Kiswahili Sanifu na katika Kitumbatu yanatokea katika mofu ya (-ta-). Lajaha ya Kitumbatu ina tabia ya kuidondosha irabu /i/ ya kiambishi nafsi (-ni-) na kusababisha mabadiliko ya maumbo ya vitenzi kutoka muundo wa ndani kwa mfano; **nitapiga, nitacheka,nitasoma** hadi muundo wa nje wa vitenzi kuwa **ntapiga, ntacheka, ntasoma.**

Kitumbatu kina tabia ya kukidondosha kiambishi awali cha nafsi ya kwanza umoja, na kukifanya kipasuo cha ufizi si ghuna kikae mwanzoni mwa kitenzi na kitamkwe kwa mpumuo. Kwa muktadha huo maumbo ya nje yatabadilika na kuunda maumbo mapya ya nje. Kwahiyo mabadiliko hayo kutoka **ntapiga** → **t̲apiga**, **ntacheka** → **t̲acheka, ntasoma** → **t̲asoma** ( **t̲**- hutamkwa kwa mpumuo). Na hii ndio tofauti kubwa na msingi iliyojitokeza baina ya Kiswahili Sanifu na Kitumbatu.

## Hitimisho

Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kwamba kuna uhusiano na muathiriano kati ya lugha hizi mbili ambapo kuna kufanana na hata kutofautiana kwa mofu (za njeo) katika matumizi kama tulivyoona katika tungo mbalimbali. Makala hii ilijikita zaidi katika vitenzi vya kawaida na kuweza kubaini mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na michakato ya kimofolojia ambayo imeathiri miundo ya vitenzi hivyo.

Ipo haja kwa watafiti kufanya uchunguzi katika vipengele vingine na vile vile Lahaja nyingine pia kama vile Kimakunduchi, Kipemba, Kiamu, Kimtang'ata, n.k..

## MAREJELEO

Crstal, D.(1997) A Dictionary of Linguistics and Phonetics (4th ed.). Oxford:Basil Blackwell.

Habwe. J na Karanja. P (2007) Misingi ya sarufi ya Kiswahili.Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.

Kapinga, C (1983) Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu. TUKI, Dar es salaam.

Kipacha .A ( 2003 ) Lahaja Za Kiswahili OSW 303. Chuo Kikuu Huria. Dar es Salaam

Mgullu,R (1988) Uhakiki wa makala ya dhana ya mofu ,alomofu, na mofimo. Mulika na.20. Dar es salaam.

Massamba na wenzake (2001) Sarufi miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA). Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba na wenzake (2003) Sarufi maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA). Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B (2002) Historia ya kiswahili 50 BK hadi 1500 BK. The Jom Kenyatta Foundation. Nairobi

Massamba, D.P.B (2004) Kiswahili cha Musoma: mwanzo wa lahaja nyingine?, journal of institute of Kiswahili Research, Vol. 9.TUKI

Martinet, A (1973) Morphonemics. New York

Mashaka H. (2017) Lulu za Isimujamii: Mtazamo wa Kisinkronia kwa Sekondari na Vyuo. Tridax Africa Company Limited. Tanzania.

https://www.researchgate.net/publication/286454770_Lahaja_Za_Kiswahili_OSW_303

http://www.mwananchi.co.tz/swahilihub/makala/2655370-2658508-885gy4/index.html